**Learning by Ear 2011 – Road Safety**

**Episode 04 - Training**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Martin Vogl**

**CHARACTERS:**

Onyesho la 1:

- ALICE (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13)
- PAMELA (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 30-40)
- NELSON (MVULANA, UMRI WA MIAKA 14)
- SAMUEL (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 30-40)
- PETER (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 60-70)

Intro/Studio/Outro:

- MTANGAZAJI BEATRICE (MWANAMKE)
- GEORGE – MTAALAMU WA USALAMA BARABARANI (MWANAMUME)

**Intro:**

**1. Beatrice:** Hujambo, jina langu ni Beatrice na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako na kipindi cha mchezo wetu wa redio. Kwenye vipindi vyetu vyote kumi tunaandamana na familia ya Wanjiru. Tunaangazia kipindi maisha yao ambapo wameshuhudia maafa yanayotokana na ukosefu wa usalama barabarani barani Afrika. Tunazungumza pia na mtaalamu wa usalama barabarani ili tujue jinsi ya kuhakikisha usalama zaidi barabarani kwa lengo la kuokoa maisha. Katika kipindi kilichopita Alice na rafiki yake, Nancy, wanahusika kwenye ajali wanapotembea barabarani. Walielewa jinsi watembeaji na madereva wanavyopaswa kutahadhari wanapotumia barabara nyakati za usiku. Katika kipindi hiki, familia ya Wanjiru imeshaungana tena nyumbani. Kwa mara ya kwanza wanajumuika na kujadiliana kuhusu mikasa waliyopata siku chache zilizopita. Mazungumzo yao yaliyotazamia kuwa na manufaa, yanageuka kuwa kulaumiana huku taarifa nyingine za kushtua zikiibuka.

**Scene One: In the family house**

**2. SFX Atmo: cooking, TV on in background**

**3. PAMELA:** Asante sana Alice kwa kutupikia chajio. Bado sijapata nguvu za kuweza kusimama kwa muda mrefu na kupika.

**4. ALICE:** Si neno, ma. Unapaswa kupumzika. Daktari alisema unahitaji majuma kadhaa kabla hujaanza tena harakati zako nyingi.

**5. NELSON:** Sasa hivi najihisi sijambo kidogo. Hata hivyo kila mara najipata nikiyawaza yaliyotendeka muda mfupi kabla ya ajali, kulikuwa na sauti ya vioo vipovunjika…

**6. PAMELA:** Ninajua unavyohisi mwanangu. Mimi pia… Si rahisi kuyasahau hivi sasa. Itachukuwa muda kiasi.

**7. NELSON:** Mama, unadhani baba anatatizwa na kumbukumbu ya mambo yaliyotokea? Hajanitajia ajali hiyo tangu sote tuliporejea kutoka hospitalini. Kwa namna fulani ninahisi kwamba yeye ndiye wa kulaumiwa kwa ajali hiyo. Bado sijamwarifu, lakini yeye ndiye aliyekuwa akiendesha gari…

**8. PAMELA:** Nelson, nadhani anachelea kukiri kwamba hakuwa mwangalifu alipokuwa akiendesha gari… Na hili mtu hulifahamu vyema hasa pale mtoto wake anapoumia. Ni jambo la kumsikitisha sana mtu. Mpe babako muda kidogo, Nelson.

**9. SFX:** **Sound of mini bus engine drawing up outside the house, doors of mini bus opening and closing**

**10. SFX:** **door of house opening, 2 people walk in**

**11. ALICE:** Shikamoo baba, shikamoo babu. Nyie wote wawili mmekuja na hilo basi?

**12. SAMUEL:** Naam.

**13. PETER:** Tumekwenda tena kwa polisi na inaonekana jamaa za abiria mmoja aliyefariki wanataka kumshtaki baba yenu mahakamani. Mvulana aliyefariki ni mtoto wa wakili mmoja tajiri anayeujua vyema mfumo wa sheria. Huenda baba yako akakabiliwa na kesi ngumu

**14. PAMELA:** Una hakika? Hilo ni jambo la kuchukua miezi na hata miaka mingi. Samuel, tutatumia mbinu gani kujipatia riziki?

**15. SAMUEL:** Sijui, Pamela. Sijui... Kusema kweli sijui tutafanya nini. Sijui nianzie wapi nimalizie wapi.

**16. SFX:** **Plates, cutlery being gathered together and put down on the table**

**17. ALICE:** Chakula tayari. Njooni mkae huku.

**18. SFX:** **Footsteps moving to the table, Chairs scraping on the floor, all the family sitting down and pulling up chairs**

**19. ALICE:** Wajua, baba. Ni vyema ukamweleza Nelson mambo yaliyotendeka… Ukizungumza na Nelson pengine hilo litakufanya uelewe hisia za familia iliyoondokewa na mtoto wao kwenye hiyo ajali.

**Silence**

**20. PETER:** Alice anasema kweli, Samuel. Sote tunaishi katika hii nyumba na hatuwezi kuyapuuza yaliyotendeka.

**21. SAMUEL:** Kwenu ni jambo rahisi sana kutwisha lawama. Lakini hapa nilipo sitawahi maishani kusahau tukio hilo.

**22. NELSON:** Lakini baba ni vyema ukiniambia yaliyotendeka! Nataka yaniondokee akili kwani yananitatiza… Nakumbuka tu lile shimo kubwa la barabarani kisha sauti za magurudumu na vigae vya vioo.

**23. SAMUEL:** Una bahati kwamba una mambo ya kukumbuka … Kuna watu chungu nzima wanaolia, damu kila mahali na hata maiti barabarani… Sitaki kukisia kwamba pengine mmoja wa hao maiti angekuwa wewe… **(almost breaking down in tears).**

**24. NELSON:** Lakini baba, Nakumbuka nilikwambia upunguze mwendo wa gari lakini ukapuuza.

**25. SAMUEL:** Najua. Hilo jambo ndilo linalonisumbua zaidi. Hata sijui kama nitaweza kuendelea kufanya kazi hii. Hata leo kuna magari yaliyokuwa yakinipita madereva wakinipigia honi kwa kuwa nilipunguza mwendo wa gari. Kusema kweli, Nelson, nimeanza kupunguza kasi. Sasa hivi ninazingatia wasemavyo abiria.

**26. ALICE:** Na vipi kuhusu mikanda ya usalama, baba? Lau ungekuwa umeiweka kwenye basi hilo jipya na ukahakikisha kwamba kila mtu amejifunga pengine hakuna abiria ambaye angejeruhiwa.

**27. SAMUEL:** Najua hivyo, Alice. Tutahakikisha kwamba tumeweka mikanda ya usalama… hilo ninakuahidi. Ninajua kwamba abiria waliokuwa kwenye gari nililoligonga walikuwa wote wamejifunga mikanda ya usalama na hakuna yeyote aliyejeruhiwa miongoni mwao…

**28. PETER:** Yote hayo yanasababishwa na jambo moja: maderva wasiokuwa na mafunzo wala uzoefu. Lau madereva wote wangetakiwa kuonesha leseni zao pengine zaidi ya nusu yao hawana hivyo vibali.

**29. ALICE:** Mtu atashikaje usukani wa gari bila kuwa na kibali cha kuendesha? Mimi huchukulia kuwa kila anayeendesha gari lazima awe na leseni. Wataka kunambia kuwa wengine hawana leseni? Si wana hatia hao?

**30. PETER:** Bila shaka wana hatia, Alice. Ndio sababu kuna ajali mbaya nyingi kama iliyompata baba yako.

**31. SAMUEL:** **(getting angry)** Sasa mnanilaumu kwa kuwa sina kibali cha kuendesha gari na tayari nimesababisha vifo vya watu wawili… Ningefanya nini na sina nafasi wala fedha za kugharamia mafunzo na kupata kibali halali? Nani atakayeisimamia familia yangu ikiwa nitaacha kazi kwa mwezi mzima eti nikafunzwe kuendesha gari vyema?

**Silence**

**32. NELSON:** Baba? **(many doubts)** Baba, una maana kwamba huna kibali halali cha kuendesha gari?

**33. PETER:** Samuel, hivi unavyosema ni kweli? Umekuwa miaka yote hiyo ukiendesha familia yako pamoja na abiria hao wote. Na huna kibali halali?

**34. SAMUEL:** Sina! **(increasingly angry)**

**35. PAMELA:** Unahisije unapoendesha gari katika barabara hizi ukijua vizuri kwamba hujui kuendesha vizuri?

**36. SAMUEL:** Lakini ninajua…

**37. PETER:** Unajua kasi inayohitajika mtu kuendesha gari barabarani?

**38. ALICE:** Na unajua kwamba mtembea kwa miguu ana haki zaidi kupita kwenye kivuko cha watembea kwa miguu?

**39. NELSON:** Hayo yote mnayoyazungmzia nimeyasoma lakini sijaona yakitekelezwa popote kwenye barabara zetu hizi. Na sasa nimejua kisa na maana. Nusu ya madereva hawajui kuendesha magari vizuri na hii ndio sababu tuna ajali zote hizo zinazoleta maafa makubwa. **(stands up)**.

**40. SFX:** **chair being pushed back**

**41. NELSON:** Siamini haya ninayoyasikia kumhusu babangu.

**42. SFX:** **Sound of stomping to the door, opening and slamming shut**

**END OF SCENE ONE**

**SHORT MUSIC**

**43. BEATRICE:** Naam, kama mlivyosiki katika hicho kipindi cha nne cha mchezo wetu wa redio kuhusu usalama barabarani, jamaa za familia ya Wanjiru wameshtuka. Studioni tunaye George, mtaalamu wetu wa usalama barabarani. Karibu George!

**44. GEORGE:** Asante.

**45. BEATRICE:** George, je umeshangazwa na hayo ambayo tumegundua – kwamba Samuel hana kibali cha kuendesha magari ilhali amekuwa kwa miaka mingi akiendesha basi lililojaa abiria?

**46. GEORGE:** Sijashangazwa na jambo hilo hata kidogo. Hii ni hali ya kawaida katika mataifa mengi barani Afrika– miji inakuwa kwa kasi kiasi kwamba usafiri wa umma unahitajika kupeleka watu wote hao kazini mwao. Hali hiyo imesababisha kuibuka biashara za matatu, mabasi na hata teksi zisizokuwa na vibali halali.

**47. BEATRICE:** Lakini ni askari polisi wanaopaswa kushughulikia tatizo hilo– wanatakikana kuchunguza vibali vya madereva?

**48. GEORGE:** Bila shaka. Polisi wanajua wanaweza kumtishia dereva asiye na kibali kwamba watamtia nguvuni na dereva anapotoa hongo anaachiliwa huru. Ni suala gumu kwa kweli.

**49. BEATRICE:** Kwa hivyo watu wanaachiwa huru kufanya watakavyo ingawa hawajajifunza taratibu za kutumia barabara?

**50. GEORGE:** Ndiyo. Katika hali hiyo hawa madereva wanasababisha vifo vya abiria wasiokuwa na hatia. Sheria zinapaswa kuzingatiwa vilivyo na magari yanatakikana kukatiwa bima na kuruhusiwa kuwa barabarani ikiwa yataendeshwa na madereva waliopewa mafunzo.

**51. BEATREICE**: Ni suala la kubadilisha mitizamo yetu. Watu wanapaswa kujizuia kabisa kuendesha magari barabarani ikiwa hawana mafunzo mwafaka na vibali vifaavyo.

**52. GEORGE:** Naam. Barani Ulaya na Marekani kuna sheria kali sana kwa watu wanaoendesha magari bila vibali. Unaweza hata kupigwa marufuku kuendesha magari au hata kupelekwa gerezani. Hatua hizo zimesaidia sana kupunguza ajali mbaya barabarani.

**53. BEATRICE:** Asante sana, George.

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**OUTRO**

**54. BEATRICE:** Katika kipindi kijacho tutasikia jinsi Samuel anavyoamua kupeleka basi lake likakaguliwe na kukarabatiwa baada ya suitafahamu kati yake na askari polisi. Endapo ungetaka kukisikiliza tena kipindi hiki, tafadhali tazama wavuti wetu www.dw.de/lbe. Asante sana kwa kujiunga nasi na jitahidi kuhakikisha usalama barabarani.